ISSN 2820-2686 | Toleo la Kumi na Moja | Aprili - Juni, 2024

# JARIDA LA WAKILI MKUU



## OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI YAPATA NAIBU WAKILI MKUU MPYA



## MAWAKILI WA SERIKALI TOENI USHAURI MAPEMA KABLA MAMBO HAYAJAHARIBIKA

# BODI YA UHARIRI


## Mwenyekiti

**Alice Edward Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Mercy Rowland Kyamba**
Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Camilius Cyprian Ruhinda**
Kaimu Mkurugenzi - Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora

**Hangi Matekeleza Chang'a**
Mkurugenzi Msaidizi - Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi

**Dennis Julius Buyekwa**
Afisa Habari

**Nkamba Josiah Mshuda**
Wakili wa Serikali

## Msanifu wa Jarida

**Nyamhoni Robert Chacha**
Afisa TEHAMA

## Wajumbe

**Salome Samuel Magesa**
Kaimu Mkurugenzi wa Usuluhishi

**Hangi Matekeleza Chang'a**
Mkurugenzi Msaidizi Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi

**Kiuye Mbwana Shemakame**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

**CPA(T) Devota Mathew Ngulugulu**
Mhasibu Mkuu

**Mercy Rowland Kyamba**
Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Zuhura Mohamed Kussaga**
Mchumi Mwandamizi

# TAHARIRI

Tarehe 04 Aprili, 2024; Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mashauri na Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Edward Mtulo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali ambapo tarehe 28 Aprili, 2024 aliapishwa.

Kuteuliwa kwa Bi. Mtulo kushika nafasi hiyo inadhihirisha kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendelea kulea na kuandaa Viongozi wanaoweza kufanya kazi kwa weledi na kuchapa kazi kwa bidii ili kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuiletea nchi yetu maendeleo.

Uteuzi huu ni ushahidi kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kuwa kioo kwa kuzalisha viongozi wanaoaminiwa na kuteuliwa na kukasimiwa majukumu ya kuendesha baadhi ya taasisi za Serikali. Hivyo, hatuna budi kuhakikisha Ofisi hii inaendelea kuwa kioo kwa taasisi nyingine za umma kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma na Serikali.

Ni imani yetu kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo ataendelea kujenga ushirikiano thabiti ulioanzishwa na watangulizi wake, kwa viongozi wa taasisi nyingine za Serikali pamoja na wadau ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mahakama ya Tanzania na taasisi mbalimbali za Serikali. Ushirikiano huu utaongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kuendelea kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wadau na umma.

Aidha, ndani ya Toleo la Kumi na Moja la Jarida la Wakili Mkuu tunakuletea makala na habari mbalimbali kuhusu uendeshaji wa mashauri yaliyomalizika ambapo mara baada ya kushinda mashauri hayo Serikali imeweza kuokoa fedha nyingi ambazo zimeelekezwa katika kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kama vile ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere, miundombinu ya barabara, vituo vya afya nchi nzima, elimu na maji ili kuendelea kuwaletea wananchi maendeleo pamoja na hayo, Jarida hili linaelezea kuhusu uendeshaji wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.



**Prisca Jackson Ulomi**
**Mhariri Mkuu**

Vile vile, toleo hili linajumuisha matukio muhimu yaliyofanyika katika kipindi chote cha toleo husika hatua ambayo itaendelea kusaidia kutoa uelewa kwa wananchi na wasomaji wetu ili waweze kuyaelewa vyema majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na namna ambavyo Ofisi imekuwa ikitekeleza majukumu yake kwa weledi kwa kuzingatia misingi ya sheria ili Taifa letu liendelee kupiga hatua za maendeleo.

Haya ni baadhi ya masuala machache yanayotarajiwa kuangaziwa katika Jarida la Wakili Mkuu Toleo la Kumi na Moja. Hivyo, kupitia ukurasa huu naomba niendelee kuwakaribisha wasomaji kutoa maoni yatakayoboresha Jarida hili ili liendelee kuwa Jarida bora na lenye mvuto kwa wasomaji. Nawatakia usomaji mwema wasomaji wetu wote wa Jarida la Wakili Mkuu Toleo la Kumi na Moja.

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



Alice Edward Mtulo
**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

Nawasilimu kwa jina la Jamhuri la Muungano wa Tanzania!

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujalia afya na uhai. Kwa nafasi ya kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Natambua dhamana hii kubwa ya uendeshaji wa Ofisi, naahidi kutumikia nafasi hii kwa weledi na uadilifu kwa kuzingatia matumizi bora ya rasilimali ili kuleta mabadiliko yenye tija na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kwa maslahi mapana ya Taifa letu.

Ili kuweza kufanikisha hayo, ni rai yangu kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali watatekeleza majukumu yao kwa weledi, uadilifu na kwa kuzingatia taratibu za utumishi wa umma.

Sambamba na hayo napenda kuwaahidi wadau wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa Ofisi itaendelea kutoa ushirikiano na kuendelea kutoa huduma bora kwa wadau wote na umma kwa ujumla.

Toleo hili la Kumi na Moja la Wakili Mkuu limebeba habari na taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Pia, wadau watapata taarifa kupitia makala zinazoeleza baadhi ya utekelezaji wa majukumu na uendeshaji wa mashauri ambayo yamemalizika na Ofisi imeweza kulinda maslahi ya Serikali na umma kwa ujumla.

Aidha, Toleo hili limebeba taarifa za shughuli mbalimbali ambazo Ofisi imefanya au imeshiriki zikiwemo ziara za Viongozi katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ushiriki wa Ofisi katika Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia, Mafunzo ya Mawakili wa Serikali, Mafunzo kwa watumishi wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ushiriki wa Ofisi katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani, ujenzi wa Ofisi kwenye Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma, na uzinduzi wa nembo ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Pia, Jarida hili limebeba makala ya watumishi katika utekelezaji wa sera zinazohusu maslahi ya watumishi ikiwemo masuala ya usalama, VVU/ Ukimwi na afya kwa ujumla. Baada ya hayo machache, napenda kuwasihi wadau wetu wote kuendelea kusoma majarida haya ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ili kuweza kupata habari na taarifa rasmi za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| UK. 06 | Rais Samia Suluhu Hassan Amteua Bi. Alice E. Mtulo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali |
| UK. 08 | Mhe. Rais Dkt. Samia Amuapisha Naibu Wakili Mkuu wa Serikali |
| UK. 11 | Zingatieni Sheria, Taratibu na Kanuni Uvunjaji wa Mikataba |
| UK. 15 | Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Waungana na Wafanyakazi Ulimwenguni Kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani |
| UK. 18 | Mawakili wa Serikali Toeni Ushauri Mapema Kabla Mambo Hayajaharibika |
| UK. 22 | Uzinduzi wa Nembo ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali |
| UK. 24 | Mawakili Wote wa Serikali Wapate Hati ya Kuendesha Mashauri Mahakamani |
| UK. 28 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yapata Hati Safi |
| UK. 30 | Tovuti Mpya Kuwapa Wadau Taarifa kwa Wakati na Yakidhi Vigezo vya eGA |
| UK. 32 | Watumishi wa OWMS Watakiwa Kupima Afya Zao Kujikinga na Magonjwa Yasiyoambukiza |
| UK. 35 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yawapiga Msasa Watumishi Wapya |
| UK. 37 | Ofisi Yashiriki Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia |
| UK. 40 | Vyanzo na Mbinu za Kuendesha na Kupunguza Mashauri ya Serikali |
| UK. 42 | Sheria Mpya za Uchaguzi na Nafasi ya Mawakili wa Serikali |
| UK. 45 | Wajibu na Majukumu ya Wakili wa Serikali |
| UK. 50 | Serikali Yashinda Mashauri Ndani na Nje Ya Nchi |
| UK. 51 | Zunda Achaguliwa Mfanyakazi Hodari wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali |



# Rais Samia Suluhu Hassan Amteua Bi. Alice E. Mtulo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali



**Bi. Alice Edward Mtulo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU

*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*

***Dar es Salaam***
***04 Aprili, 2024***

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi na utenguzi wa viongozi kama ifuatavyo:

i) Amemteua Mhe. Jaji Winfrida Beatrice Korosso kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT). Mhe. Jaji Korosso ni Jaji wa Mahakama ya Rufani.

ii) Amemteua Bi. Bibiana Joseph Kileo kuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Kabla ya uteuzi huu Bi. Kileo alikuwa Mkuu wa Mashtaka Mkoa (RPO), Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Mwanza.

iii) Amemteua Bi. Alice Edward Mtulo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Kabla ya uteuzi huu, Bi Mtulo alikuwa Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Kesi na Udhibiti Ubora, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

iv) Ametengua uteuzi wa Bi. Catherine Michael Mashalla, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz

S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

29 Aprili, 2024

**MHE. RAIS DKT. SAMIA AMUAPISHA NAIBU WAKILI MKUU WASERIKALI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amemuapisha Bi. Alice Mtulo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali kwenye hafla iliyofanyika tarehe 28 Aprili, 2024 kwenye viwanja vya Ikulu Jijini Dar es Salaam.

Uapisho huo umeshuhudiwa na Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini; Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bi. Mary Makondo; Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi; Mkurugenzi wa Mashtaka, Sylvester Mwakitalu na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende. Mara baada ya uapisho huo viongozi hao walikutana pamoja kwenye ukumbi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam kumpokea Bi. Mtulo na kumpa nasaha za kumtakia mema katika majukumu yake mapya.

Mhe. Sagini alimueleza Bi. Mtulo kuwa utendaji kazi wa pamoja na ushirikiano ni muhimu ili kufanikisha mnyororo wa haki jinai ili sote tuweze kuwahudumia watanzania. Naye Bi. Makondo alisema kuwa anamshukuru Mhe. Rais Samia kwa kuwateua na kuwaapisha viongozi watatu wa taasisi za Wizara hiyo akiwemo Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Mhe. Jaji Winfrida Korosso; Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bibiana Kileo; na Bi. Alice Mtulo, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwa viongozi hao watasimamia utendaji kazi wa Ofisi zao.

Mhe. Feleshi amewaeleza kuwa uteuzi wao ni wa kuaminiwa na kuwezeshwa na wengine hivyo watambue wana dhamana kubwa ya uendeshaji wa Ofisi na amewataka wasisahau majukumu ya msingi ya Ofisi zao na wawe tayari kuleta mabadiliko katika utendaji.

Naye Dkt. Luhende ameahidi kuwapa ushirikiano viongozi hao wapya na amewasihi kuomba ushauri pale inapobidi kwa kuwa utumishi wa umma unahitaji hivyo na washirikiane kwa pamoja kwa maslahi mapana ya Taifaletu. Ndugu Mwakitalu aliwaeleza kuwa nafasi zao za uteuzi zinahusu watumishi na wananchi na wote wanasubiri huduma yao.

Bi. Mtulo aliwashukuru viongozi kwa kumpokea na kwa nasaha zao na kwa kumlea hivyo ameomba waendelee kufanya kazi kwa bidii ili kufanikisha haki jinai nchini.

Imetolewa na:

Prisca J. Ulomi
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Bi. Alice Mtulo kuwa Naibu Wakili Mkuu wa Serikali. Katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam tarehe 29 Aprili, 2024.*



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini akizungumza na viongozi wa taasisi za Wizara ya Sheria na Katiba na baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara baada ya kuwakaribisha na kuwapokea Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo; Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Bi. Bibiana Kileo; na Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Mhe. Jaji wa Mahakama ya Rufani Winfrida Korosso (hawapo pichani) katika mapokezi yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dar es Salaam tarehe 29 Aprili, 2024.*

*Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akimkaribisha Mhe. Jumanne Sagini (Mb) ili azungumze na viongozi wa taasisi za Wizara hiyo (hawapo pichani) mara baada ya kuwakaribisha na kuwapokea Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo; Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Bi. Bibiana Kileo; na Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Mhe. Jaji wa Mahakama ya Rufani Winfrida Korosso katika mapokezi yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dar es Salaam tarehe 29 Aprili, 2024..*



*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na viongozi wa Taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) mara baada ya kuwakaribisha na kuwapokea Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo na Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Mhe. Jaji wa Mahakama ya Rufani Winfrida Korosso kwenye ukumbi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam tarehe 29 Aprili, 2024.*





*Naibu Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo akizungumza na viongozi wa Taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) mara baada ya kuapishwa.*



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi akizungumza na viongozi wa Taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) mara baada ya kuwakaribisha na kuwapokea Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo na Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria Mhe. Jaji wa Mahakama ya Rufani Winfrida Korosso katika mapokezi yaliyofanyika kwenye ukumbi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini (Mb) akizungumza na Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (hawapo pichani) wakati wa ziara yake ya kikazi kwenye Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam.*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz

S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

## *ZINGATIENI SHERIA, TARATIBU NA KANUNI UVUNJAJI WA MIKATABA*

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini amezitaka Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kuzingatia sheria, kanuni na taratibu katika hatua za uvunjaji wa mikataba iliyoridhiwa kwa ajili ya utekelezaji

Mhe. Sagini ameyasema hayo wakati wa ziara yake alipotembelea Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) jijini Dar es Salaam na kuzungumza na menejimenti ya Ofisi hiyo kwa lengo la kujifunza, kufahamu majukumu na utendaji kazi, mafanikio na changamoto za Ofisi hiyo ili Wizara iweze kuzifanyia kazi kwa maslahi mapana ya Serikali na manufaa ya taifa letu

Ameyasema hayo baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji ya

Ofisi hiyo iliyowasilishwa kwake na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende ambapo aliarifiwa kuwa Ofisi hiyo inaendesha mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake na kwenye taasisi binafsi ambapo Serikali ina hisa.

Aidha, Mhe. Sagini ameielekeza OWMS kuandaa taarifa ya Wizara na taasisi za Serikali zinazovunja mikataba bila kuzingatia sheria, taratibu na kanuni ili ziweze kufanyiwa kazi na kupunguza mashauri ya Serikali yaliyopo mahakamani

Katika hatua nyingine Mhe. Sagini ***ameipongeza OWMS kwa kuendesha na kushinda mashauri ya Serikali ndani na nje ya nchi ikiwemo shauri la ujenzi wa bomba la mafuta la kutoka Hoima-Uganda hadi Chongoleani-Tanga; uendeshaji wa bandari kupitia kampuni ya DP World; ununuzi wa mafuta wa pamoja; na Jaji Mkuu wa Tanzania kuongezewa muda ni sahihi kikatiba ambapo mashauri hayo yameendeshwa na Mawakili wa Serikali wa OWMS.***

Akiwasilisha taarifa ya OWMS, Dkt. Luhende alimuarifu Mhe. Sagini kuwa zipo baadhi ya changamoto ambazo zinasababisha Serikali na taasisi zake kushitakiwa mahakamani ikiwemo ***uvunjaji wa mikataba bila kuzingatia sheria, taratibu na kanuni; uvunjaji wa mikataba bila kuishirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; ushirikiano hafifu wa kupata nyaraka za kuendeshea mashauri mahakamani; migogoro ya ardhi ikiwemo masuala ya utwaaji wa maeneo, upimaji, ulipaji fidia, na ugawaji viwanja; ucheleweshaji wa kufanyia kazi malalamiko ya wawekezaji; na kuchelewesha malipo ya wakandarasi.***

Pia, Mhe. Sagini amempongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utashi wake wa kisiasa wa kuiendeleza na kuiwezesha Ofisi hiyo kutekeleza majukumu yake, ***"nimefarijika kwa kupokea ripoti yenye mafanikio mengi kuliko changamoto, Ofisi ina muda mfupi, mmepiga hatua kubwa kwa kushughulika na kesi za madai na usuluhishi, sasa Serikali ina watu ambao wakilala na kuamka wanawaza uendeshaji wa kesi tu."***

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo ameishukuru Serikali kwa kuiongezea bajeti Ofisi hiyo ya kutekeleza majukumu yake kutoka shilingi bilioni 17 Mwaka wa Fedha 2023/24 na kufikia shilingi bilioni 20 kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 na Ofisi iko tayari kushirikiana na Wizara kufanikisha utekelezaji wa majukumu na hadi sasa Ofisi ipo kwenye mikoa 17 na itaendelea kufungua Ofisi kwenye mikoa mbali mbali nchini ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Imetolewa na:

Prisca J. Ulomi
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
11 Mei, 2024



*Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende akifafanua jambo kwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini (Mb), (hayupo pichani) wakati wa ziara yake kwa viongozi na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini (Mb) akipitia kitabu cha mkusanyiko wa sheria mbalimbali alipotembelea Maktaba ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara yake ya kikazi kwenye Ofisi hiyo Jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini (Mb), (kushoto) akipokea kitabu chenye jumbe za ukaribisho kutoka kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara baada ya kuzungumza na watumishi hao alipotembelea Ofisi hiyo wakati wa ziara yake ya kikazi Jijini Dar es Salaam. Anayemkabidhi kitabu hicho ni Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende.*



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini (Mb), (wa pili kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Masjala ya Sheria ndugu Dennice Leonard namna Mfumo wa Usimamizi wa Mashauri ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali unavyofanyakazi wakati wa ziara yake kwenye Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam.*



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini (Mb), (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya viongozi na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa ziara yake kwenye Ofisi hiyo jijini Dar es Salaam.*



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango akizungumza na watumishi na wananchi walioshiriki Maadhimisho ya Siku ya Wanyakazi Duniani yaliyofanyika kitaifa Katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid mkoani Arusha. Makamu wa Rais amemwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Maadhimisho hayo.*

# Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Waungana na Wafanyakazi Ulimwenguni Kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali tarehe 01 Mei, 2024 waliungana na wafanyakazi wenzao kote ulimwenguni kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani. Mgeni Rasmi wa maadhimisho hayo alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango aliyemwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza mara baada ya Maadhimisho hayo, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ndugu James Kibamba amesema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inajivunia mafanikio na mchango mkubwa uliotolewa na watumishi wa Ofisi hiyo katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku ambayo ni kusimamia, kuratibu

na kuendesha mashauri yote ya madai na usuluhishi ili kuhakikisha nchi inaendelea kupiga hatua za maendeleo katika sekta mbalimbali.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa TUGHE Tawi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ndugu Mtani Songorwa amesema kuwa Maadhimisho hayoyanasaidia kwa kiasi kikubwa kuitangaza Ofisi kwa wananchi ili waweze kufahamu majukumu yake na namna ambavyo imekuwa ikiendesha mashauri ya Serikali kwa weledi na ufanisi mkubwa.

Ameongeza kuwa faida nyingine ya kushiriki Maadhimisho hayo ni kujenga mahusiano mazuri kati ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Taasisi nyingine za Serikali ikiwemo vyama vya wafanyakazi kutoka sekta mbalimbali.

Maadhimisho ya Mei Mosi Kitaifa yamefanyika katika Viwanja wa Sheikh Amri Abeid vilivyopo jijini Arusha yakiwa yamebeba kauli mbiu isemayo, "Nyongeza ya Mishahara ni Msingi wa Mafao Bora na kinga Dhidi ya Hali Ngumu ya Maisha."




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango akiwasalimia wafanyakazi mbalimbali waliojitokeza katika Sherehe za Mei Mosi wakati akiwasili katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid mkoani Arusha kushiriki Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani tarehe 01 Mei 2024.*




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango akisalimiana na viongozi mbalimbali wakati akiwasili katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid mkoani Arusha kushiriki Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani tarehe 01 Mei 2024. Makamu wa Rais amemwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Maadhimisho hayo.*

*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ndugu James Kibamba (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Ofisi hiyo baada ya Sherehe za Maadhimisho ya Mei Mosi zilizofanyika katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid Mkoani Arusha.*






*Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango (hayupo pichani) wakati akizungumza na watumishi na wananchi walioshiriki katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika kitaifa Katika uwanja wa Sheikh Amri Abeid mkoani Arusha.*




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz

S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

## MAWAKILI WA SERIKALI TOENI USHAURI MAPEMA KABLA MAMBO HAYAJAHARIBIKA

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini amewataka Mawakili wa Serikali kutoa ushauri mapema kabla mambo hayajaharibika. Ni vema mtoe ushauri mapema pale ambapo mnaona jambo lina dalili ya kuharibika kwa kushauri vema viongozi wa taasisi zao ili kuiepusha Serikali na taasisi zake kuzalisha mashauri na migogoro mbali mbali nchini.

Hayo yameelezwa na Mhe. Sagini wakati akifungua mafunzo kwa Mawakili wa Serikali zaidi ya mia tano yaliyopangwa kufanyika kwa siku tatu jijini Arusha kuanzia tarehe 20 Mei, 2024. Pia, alizindua nembo ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa

*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini (Mb) akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati akifungua mafunzo ya siku tatu kwa mawakili wa serikali yanayofanyika jijini Arusha.*

Serikali ambayo imechapishwa kwenye Gazeti la Serikali Toleo Na. 19 la tarehe 10 Mei, 2024 na iko tayari kuanza kutumika. Mhe. Sagini alifungua mafunzo hayo na kuzindua nembo hiyo kwa niaba ya Waziri wa Wizara hiyo, Mhe. Dkt. Balozi Pindi Chana.

Aliongeza kuwa ***matarajio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mawakili wa Serikali baada ya kupata mafunzo hayo ni kuwa chachu katika usimamizi na utatuzi wa migogoro ya mikataba inayotokana na Sekta ya Ujenzi kwani nchi yetu ipo kwenye ujenzi wa miradi mikubwa ya kimkakati; kuwa chachu katika kupunguza na kutatua migogoro ya uwekezaji katika Sekta ya Madini na rasilimali za nchi; kupunguza idadi ya mashauri ya madai na usuluhishi yanayofunguliwa na yanayoendelea kwa kuyamaliza kwa njia ya usuluhishi hivyo kuimarisha juhudi za Serikali katika kuvutia wawekezaji na kutekeleza miradi mbali mbali nchini; kuwashauri waajiri ipasavyo kuhusiana na taratibu za uendeshaji wa mashauri ya nidhamu pale wanapohitajika kuchukua hatua za nidhamu dhidi ya watumishi wa umma; kuishauri ipasavyo Serikali na taasisi zake wakiwemo viongozi wa ngazi mbalimbali kuhusu namna bora ya kumaliza migogoro na wananchi au wawekezaji bila kuathiri maslahi ya nchi; na kusimamia na kuendesha vizuri mashauri ya uchaguzi yatakayofunguliwa kabla na baada ya uchaguzi mkuu pamoja na uchaguzi wa Serikali za Mitaa***

Akizungumza wakati wa akimkaribisha Mgeni Rasmi Mhe. Sagini, Wakili Mkuu wa Serikali Dkt. Boniphace Luhende alisema kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuendelea kuwanoa Mawakili wa Serikali ili kuboresha utendaji kazi wao; kupunguza ongezeko la mashauri kwenye baadhi ya maeneo yanayozalisha migogoro mingi dhidi ya Serikali ambapo hadi kufikia Mwezi Aprili, 2024 Ofisi ***imeendesha jumla ya mashauri 7,813 na kati ya hayo mashauri ya ndani ni 7,798 na mashauri ya nje ya nchi ni 15 na kati ya mashauri hayo, mengi yametokana na migogoro ya ardhi, kazi, mikataba, manunuzi, bima, Katiba na haki za binadamu.***

Aidha, Ofisi imeendesha jumla ya mashauri ya usuluhishi 179 na kati ya hayo mashauri 148 ni ya ndani ya nchi na mashauri 31 ni ya nje ya nchi na mengi yametokana na mikataba ya ujenzi, uwekezaji na taratibu za manunuzi. Vile vile, Ofisi imeshughulikia notisi za siku 90 zipatazo 723 zilizowasilishwa katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Aprili, 2024 na asilimia kubwa ya notisi hizo zinahusu masuala ya ardhi, kazi na mikataba ambayo taasisi za Serikali zimeingia na wadau mbalimbali.

Pia, Dkt. Luhende aliongeza kuwa tangu Ofisi imeanza kufanya mafunzo hayo wameshuhudia ongezeko la ubora wa kazi zinazotekelezwa na imeiwezesha Ofisi kuwa na mafanikio mbali mbali ikiwemo ***Serikali kushinda mashauri ya madai 743 yenye thamani ya shilingi bilioni 406.4 na mashauri 15 ya usuluhishi yenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 1.5.***

Aidha, Ofisi imeendesha na kushinda mashauri yenye umuhimu mkubwa kwa ustawi wa taifa letu ambayo ni ***shauri la ujenzi wa mradi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganda mpaka Chongoleani – Tanga ambapo Serikali ingeshindwa mradi huu wenye takribani shilingi trilioni 8 usingeweza kutekelezwa; mkataba wa uwekezaji wa Bandari ya Dar es Salaam na uwekezaji wa kiwanda cha saruji Tanga na iwapo Serikali ingeshindwa uwekezaji huo usingeweza kufanyika; na kushinda shauri la usuluhishi la kimataifa lenye lenye takriban shilingi bilioni 36 baina ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC kupitia uamuzi wa Baraza la Kimataifa la Biashara (ICC).***

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo alisema kuwa mafunzo hayo ni muendelezo wa mipango ya Ofisi hiyo ya kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali wa Ofisi

hiyo na waliopewa hati idhini ya kuendesha mashauri kwa niaba ya Ofisi hiyo. Amefafanua kuwa mafunzo hayo yanajumuisha washiriki kutoka kwenye Wizara, taasisi, mashirika ya umma, mamlaka za Serikali za Mitaa, tume, vyuo vikuu, mabenki na bodi mbali mbali pamoja na washiriki kutoka Zanzibar.

Aidha, ameongeza kuwa mafunzo hayo yatatolewa na wakufunzi kumi na moja wabobezi ambao ni Majaji na Majaji wastaafu kutoka Mahakama Kuu ya Tanzania, wanataaluma na wataalam wabobezi wa Sekta ya Sheria nchini, wakufunzi kutoka vyuo vikuu nchini na wataalamu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Imetolewa na:

Prisca J. Ulomi
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
21 Mei, 2024

*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akitoa salamu za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati akimkaribisha Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini (Mb) (hayupo pichani) ili afungue mafunzo ya siku tatu kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.*





*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) wakati wa mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Arusha.*



*Mawakili wa Serikali walioshiriki Mafunzo wakimsikiliza Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini (Mb) (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika jijini Arusha.*



*Mawakili wa Serikali walioshiriki Mafunzo ya siku tatu wakimsikiliza Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini (Mb) (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo hayo yaliyofanyika jijini Arusha.*




*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Prisca Ulomi akitoa maelezo kuhusu nembo ya Ofisi hiyo muda mfupi kabla ya uzinduzi wa nembo hiyo uliofanyika Jijini Arusha.*







*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini (Mb) (katikati) akizindua nembo ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kufungua mafunzo ya Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.*

Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini (Mb), alizindua Nembo ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali tarehe 20 Mei, 2024 sambasamba na ufunguzi wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha. Nembo hiyo imechapishwa kwenye Gazeti la Serikali Toleo Na. 19 la tarehe 10 Mei, 2024 na iko tayari kuanza kutumika.

Nembo hiyo imebeba na kujumuisha vielelezo mbalimbali ambavyo vinaakisi majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ya uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
OFFICE OF THE SOLICITOR GENERAL
OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# NEMBO YA OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Person + Scales + Constitution + Pen + Jabot



**KEY**

Person - An Authoritative figure that represents leadership.

Scales - A symbol of Justice or balance.

Constitution - Every legal execution is result of written references that act as Guiding Legal writings.

Pen - A legal tool of work. For anything to be legally bounded it has to be spelt out. A pen is just a tool for that.

Jabot - Legal attire.




*Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Arusha.*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

Simu: +255 22 2127384
Nukushi: +255 22 2127384
Tovuti: www.osg.go.tz
Barua Pepe: info@osg.go.tz

S.L.P 71554
10 Barabara ya Kivukoni
11405 Dar es Salaam
TANZANIA

## MAWAKILI WOTE WA SERIKALI WAPATE HATI YA KUENDESHA MASHAURI MAHAKAMANI

Mawakili wote wa Serikali nchi nzima wa Ofisi zote za Serikali wapatiwe hati ya kuendesha mashauri ya Serikali mahakamani kwa niaba ya Serikali.

Hayo yamesemwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dkt. Balozi Eliezer Feleshi alipokuwa

anafunga mafunzo ya siku tatu kwa Mawakili wa Serikali yaliyomalizika tarehe 22 Mei, 2024 yaliyoandaliwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.

Dkt. Feleshi amemuelekeza Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende kutoa mwongozo kwa Mawakili wote wa Serikali wa Wizara, taasisi na idara za Serikali ili wote waende mahakamani katika maeneoyaoyakaziwalipokwakuwakutokwendamahakamaninikuletaukinzani baina ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

***"Wakili wa Serikali unapoenda mahakamani utoe mrejesho kwa aliyekutuma na tukumbuke tumepewa hati ya kuendesha mashauri ya Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali ya Kwenda mahakamani kuendesha mashauri hivyo tuitendee haki nafasi hiyo na tutoe taarifa kwa Wakili Mkuu wa Serikali, amesema Dkt. Feleshi."***

Ameongeza kuwa anaelewa Mawakili wa Serikali wamepatiwa elimu ya msingi ya sheria za uchaguzi ambapo kanuni zake zipo mbioni kutoka hivyo, amewataka Mawakili hao wajiandae kuzisoma na kuzielewa na pale itakapohitajika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itoe nafasi ya kuwapa uelewa wa kanuni hizo.

***"Sisi tuwe sehemu ya kuhakikisha chaguzi zote ziwe za haki, zifuate sheria, taratibu na kanuni na zizingatie 4R za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muunngano wa Tanzania."***
Aidha, amewataka Mawakili hao kufahamu kuwa Mawakili wa Serikali ni akili ya Serikali. Hivyo, hategemei kuona Wakili wa Serikali akiendesha mashauri bila kujali anaendesha kwa niaba ya Serikali na aendeshe kwa viwango stahiki, ajitafakari, na kujitathmini pale ambapo tunapoteza kesi sehemu ambayo tulistahili tushinde. Muhimu tufuate taratibu zote mpaka tushinde kesi, amesisitiza Dkt. Feleshi.
Akimkaribisha Dkt. Feleshi kufunga mafunzo hayo, Dkt. Luhende amesema kuwa mafunzo yaliyotolewa kwa Mawakili wa Serikali yatapunguza migogoro iliyopo na mada zilizotolewa zilichaguliwa kutokana na uzoefu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilioupata katika kuendesha mashauri ya Serikali.

***"Jeshi huandaliwa wakati wa amani, hivyo Mawakili wa Serikali wamepatiwa mafunzo kuhusu sheria za uchaguzi wa Serikali za mitaa na uchaguzi mkuu," amefafanua Dkt. Luhende.***

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo, amewashukuru waajiri wote wa Serikali kwa kuwapatia ruhusa Mawakili kushiriki mafunzo hayo na amewaomba waendelee na moyo huo ili kuendelea kuwanoa Mawakili hao.Aidha, amewashukuru wafadhilikwa ushirikiano na mshikamano katika kufanikisha mafunzo hayo.

Mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo, Bi. Nuru Pipino, Afisa Sheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji amesema kuwa mafunzo hayo yamekuwa chachu kwake na yatawawezesha kuendesha mashauri ya Serikali na wamepata uelewa wa sheria za uchaguzi.

Imetolewana:

PriscaJ.Ulomi
**Mkuuwa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

22 Mei, 2024




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) wakati akimkaribisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi afungue mafunzo kwa Mawakili wa Serikali hao yaliyofanyika jijini Arusha.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Alice Mtulo akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) wakati wa kufunga mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Arusha.*




*Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Robert Makaramba, akitoa mada kuhusu taratibu za uendeshaji wa Mashauri ya Mahakama ya Rufani wakati wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.*



*Waziri wa Katiba na Sheria Mstaafu, Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi (Mb) akitoa mada kuhusu masuala ya kuzingatia katika uendeshaji mashauri ya Serikali wakati wa mafunzo ya Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.*

*Mawakili wa Serikali wakiwasikiliza wawezeshaji wa mada zilizotolewa wakati wa mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofayika Jijini Arusha.*



> *“Wakili wa Serikali unapoenda mahakamani utoe mrejesho kwa aliyekutuma na tukumbuke tumepewa hati ya kuendesha mashauri ya Serikali na Wakili Mkuu wa Serikali ya Kwenda mahakamani kuendesha mashauri hivyo tuitendee haki nafasi hiyo na tutoe taarifa kwa Wakili Mkuu wa Serikali, amesema Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali.”*

# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yapata Hati Safi



**CPA(T) Devota Ngulugulu**
*Mhasibu Mkuu*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kupata Hati Safi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kipindi cha miaka mitano (05) mfululizo tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018. Mwaka wa Fedha 2022/23, Ofisi ilitengewa bajeti ya jumla ya shilingi 12,812,816,000.

Ofisi hii imefanya matumizi ya fedha tajwa kuendana na mgao wa fedha wa kila mwezi unaowasilishwa kutoka HAZINA na kuiewezesha Ofisi kutekeleza majukumu ya msingi ya uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ya ndani na nje ya nchi pamoja na majukumu ya uendeshaji wa Ofisi, mafunzo ya kuwajengea uwezo na utaalam watumishi, ununuzi wa vitendea kazi kama vile magari, kompyuta, kuweka mazingira bora na wezeshi kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi na miundombinu mathalani mifumo ya TEHAMA.

Upatikanaji wa Hati Safi umetokana na dhana ya uwajibikaji wa pamoja na uwazi uliopo baina ya Menejimenti na watumishi wa Ofisi ambapo fedha zinatengwa na kuridhiwa matumizi baada ya kufanyika kwa kikao cha Kamati ya Bajeti ya kila mwezi kwa ajili ya kujadili mgao wa fedha iliyopokelewa ambacho huratibiwa na Idara ya Mipango. Wajumbe wa kikao hicho ni Wakuu wa Idara na Vitengo wenye kasma na vifungu vyenye majukumu na tengeo la fedha kama ilivyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa


Tanzania kwa kuzingatia Mpango Kazi ulioidhinishwa.

Aidha, katika kuhakikisha matumizi stahiki ya fedha na utekelezaji wa majukumu, Ofisi imejiwekea utaratibu wa kufanya vikao vya kila wiki kwa Idara za Sheria Idara na Vitengo wezeshi ili kujadili masuala yanayohusu ufanisi na muono mbele katika kushughulikia mashauri na majukumu ambayo yanahitajika kutekelezwa kwa ufanisi na kwa muda muafaka kwa lengo la kuwawezesha watumishi wa Idara mama kutekeleza majukumu ipasavyo ikiwa ni pamoja na mazingira wezeshi ya utendaji kazi.

Vile vile, Ofisi inazingatia maelekezo ya sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya fedha inayotolewa kila mwaka yenye maelekezo ya matumizi ya fedha kwa Idara na taasisi za Serikali ili kuhakikisha matumizi hayo yanakuwa na tija, ufanisi na kuakisi mahitaji ya wananchi na malengo ya Serikali kwa ujumla.

Pia, uwepo wa mifumo inayosimamia na kudhibiti matumizi ya fedha za umma ambayo ni pamoja na uwepo wa Kamati ya Ukaguzi, Kitengo cha Ugavi na Manunuzi, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani na mifumo ya malipo ya Serikali (MUSE) inayotumia TEHAMA. Uwepo wa mifumo hiyo inabeba jukumu la kuwa jicho la Afisa Masuuli na taasisi kwa ujumla ili kuhakikisha kuwa matumizi ya fedha yanaendana na majukumu yaliyopangwa kutekelezwa; yanazingatia sheria ya fedha na Sheria ya manunuzi na matumizi sahihi ya kasma na vifungu vya bajeti kwa mujibu wa mpango kazi wa Ofisi.

Aidha, kumekuwepo na ushirikishwaji wa wafanyakazi kupitia vikao vya Baraza la Wafanyakazi na Mkutano Mkuu wa mwaka wa watumishi wote ambapo wajumbe hupata fursa ya kupitia mipango, majukumu na utekelezaji wake ili kuhakikisha kuwa Ofisi inafikia malengo iliyojiwekea ya kuiwakilisha Serikali na taasisi zake kwenye mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi. Hivyo, ni matumaini ya Kitengo cha Uhasibu na Fedha kuwa dira na azma iliyowekwa itaendelea kutimizwa ili Ofisi iendelee kupata hati safi. Kongole kwa Afisa Masuuli, Menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kupata hati safi!



REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

NATIONAL AUDIT OFFICE

OFFICE OF SOLICITOR GENERAL

REPORT OF THE CONTROLLER AND AUDITOR GENERAL ON THE FINANCIAL AND COMPLIANCE AUDIT FOR THE FINANCIAL YEAR ENDED 30 JUNE 2023

Controller and Auditor General,
National Audit Office,
Audit House,
4 Ukaguzi Road,
P.O. Box 950,
41101 Tambukareli,
Dodoma, Tanzania.
Tel: 255 (026) 2161200,
Fax: 255 (026) 2117527,
E-mail: ocag@nao.go.tz
Website: www.nao.go.tz

February 2024

AR/CG/19/OSG/2022/23



1.2.2 Compliance with the Budget Act and other Budget Guidelines

Subject matter: Budget formulation and execution
I performed a compliance audit on budget formulation and execution in the Office of Solicitor General for the financial year 2022/23 as per the Budget Act and other Budget Guidelines.


Conclusion
Based on the audit work performed, I state that Budget formulation and execution of the Office of Solicitor General is generally in compliance with the requirements of the Budget Act and other Budget Guidelines.

Charles E. Kichere
Controller and Auditor General,
Dodoma, United Republic of Tanzania

February 2024

Controller and Auditor General AR/CG/19/OSG/2022/23 5

# Tovuti Mpya Kuwapa Wadau Taarifa kwa Wakati na Yakidhi Vigezo vya eGA




*Muonekano wa Tovuti Mpya ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeboresha tovuti yake ili iwe ya kisasa zaidi hatua itakayovutia wadau wake na wananchi kwa ujumla ambao wamekuwa wakitembelea tovuti hiyo kwa lengo la kupata taarifa mbalimbali zinazohusu Ofisi hiyo.

Akizungumza mara baada ya mafunzo kuhusu upakiaji wa taarifa kwenye tovuti mpya kwa watumishi wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini na Kitengo cha TEHAMA wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Bi. Prisca Ulomi amesema kuwa uamuzi wa kuboresha tovuti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali umekuja muda muafaka kwa kuwa tovuti mpya itaitangaza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuwapatia wadau hao taarifa sahihi na kwa wakati.

Akizitaja faida za kukamilika kwa tovuti hiyo, Bi. Ulomi amesema kuwa uwepo wa tovuti hiyo utasaidia kwa kiasi kikubwa kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu namna Ofisi inavyotekeleza majukumu yake na kuwapa wananchi fursa za kuyafahamu majukumu hayo hatua itakayoongeza wigo zaidi wa kuwafikia wananchi kwa haraka tofauti na kutumia njia nyingine kama vile vipeperushi ambapo njia hii itawafikia wadau wachache.

Alieleza kuwa kupitia Tovuti hiyo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itapata nafasi ya kueleza, kutangaza na kufikisha ujumbe wake kwa wadau wengi zaidi wa ndani na nje ya nchi kwa kuwa pamoja na uwepo wa mitandao ya kijamii watu wengi bado wanaamini zaidi taarifa zinazopatikana kwenye tovuti rasmi za taasisi za Serikali.

Aliongeza kuwa tovuti hii mpya itawapatia wananchi nafasi ya kupata taarifa mbalimbali ikiwemo makala za kuelimisha na kuvutia wadau wake ili waweze kufahamu majukumu yanayotekelezwa na Ofisi ambayo ni pamoja na Ofisi kuwa kiungo muhimu katika kuokoa fedha nyingi ambazo zingelipwa kama Serikali ingeshindwa mashauri Mahakamani ambapo sasa Serikali inatumia fedha hizo kujenga miradi mikubwa ya maendeleo kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Akifafanua namna wadau wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali watakavyonufaika na tovuti hiyo, Bi. Ulomi amesema kuwa kupitia tovuti hiyo wafuatiliaji wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali watapata fursa ya kupata taarifa nyingi zaidi tofauti na tovuti ya zamani ambayo ilikuwa na uwezo wa kubeba taarifa chache kwa sababu ya teknolojia iliyotumika kujenga tovuti hiyo ni ya zamani hivyo hairuhusu kubeba taarifa nyingi.

Tovuti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imejengwa na wataalamu wa ndani kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ambapo baada ya kukamilika, wataalam wa eGA waliendesha mafunzo kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ya namna ya kuweka maudhui kwenye tovuti hiyo. Mafunzo hayo yalifanyika katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere kilichopo Kibaha Mkoani Pwani.





*Ndugu Mtani Songorwa, Katibu Sheria wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali akipima afya baada ya kupata elimu ya afya na upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza, VVU/UKIMWI wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali uliofanyika Jijini Arusha.*

# Watumishi wa OWMS Watakiwa Kupima Afya Zao Kujikinga na Magonjwa Yasiyoambukiza

Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wametakiwa kujenga tabia ya kupima afya zao kila wakati ili waweze kupata ushauri sahihi kuhusu namna ya kujikinga na magonjwa sugu yasiyoambukiza na VVU.

Wito huo umetolewa na Mratibu wa kudhibiti VVU na magonjwa yasiyoambukizwa kutoka Hospitali ya Wilaya ya Arusha, Dkt. Japhet Champanda wakati akitoa elimu kuhusu VVU/UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza kwa watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.

Dkt. Champanda alieleza kuwa kupima afya mara kwa mara itawasaidia watumishi hao kufahamu hali ya afya zao ikiwa ni pamoja na kupata elimu sahihi ya masuala ya afya itakayowasaidia kujikinga na magonjwa hayo sambamba na kubadili mtindo wa maisha kwa watumishi hao.

Amesisitiza kuwa uamuzi wa watumishi kupima afya zao kutawasaidia kwa kiasi kikubwa kujiepusha na magonjwa sugu kama vile kisukari, shinikizo la damu, kiharusi, ugonjwa wa figo na ini.

Mtaalam wa afya kutoka Hospitali ya Wilaya ya Arusha amewashauri watumishi hao pia waendelee kufuatilia taarifa sahihi za namna ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza na yanayoambukiza kama vile VVU/UKIMWI ili kupata taarifa sahihi ili waweze kusaidia kutoa elimu ya kujikinga na maradhi hayo kwa wananchi na jamii kwa ujumla.

Akizungumza wakati wa zoezi la upimaji afya kwa watumishi hao, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili mkuu wa Serikali, ndugu James Kibamba amesema kuwa zoezi la upimaji wa afya ni muhimu kwa watumishi waliopo kwenye Ofisi hiyo kutokana na watumishi kukosa muda wa kuchunguza afya zao katika vituo vya afya kutokana na kuwa na majukumu mengi.

Ndugu Kibamba alieleza kuwa wameamua kuendesha zoezi la upimaji wa afya kwa watumishi kwa kuzingatia ukweli kuwa mtumishi akiwa na afya njema atatekeleza majukumu yake kwa ufasaha na hivyo kuisaidia Ofisi kufikia malengo iliyojiwekea kuendana na Mpango Kazi wake.

Kwa upande wake Mratibu wa zoezi hilo ndugu Geofrey Annaniah alisema kuwa watumishi wanatakiwa kupima afya zao ili waweze kufahamu namna ya kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza kwani limekuwa janga kwa jamii kwa sababu ya kukosa muda wa kufanya mazoezi, kupima afya zao na mtindo wa maisha usiofaa.

Wakizungumza mara baada ya kupima afya zao baadhi ya watumishi walioshiriki zoezi hilo waliishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuendesha zoezi hilo kwa kuwa limewawezesha kupata nafasi ya kujua hali ya afya zao na sasa wataweza kuishi kwa kuchukua tahadhari kulingana na maelekezo na ushauri walipata kutoka kwa wataalam wa afya.


Mbali na kuendesha zoezi la kupima afya za watumishi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilitoa elimu kuhusu afya ya akili kwa watumishi wake iliyotolewa na Dkt. Garvin Kweka wa Hospitali ya Taifa Muhimbili akishirikiana na Dkt. Aisha Zukheri kutoka Ofisi ya Mganga Mkuu wa Jiji la Dar es Salaam aliyetoa elimu kuhusu VVU na UKIMWI.



*Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Nicodemus Agweyo akipima afya baada ya kupata elimu ya afya na upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza, VVU na UKIMWI wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa watumishi wa Ofisi hiyo uliofanyika Jijini Arusha.*




*Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Francis Wisdom akipima afya baada ya kupata elimu ya afya na upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza, VVU na UKIMWI wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa watumishi wa Ofisi hiyo uliofanyika Jijini Arusha.*



*Afisa TEHAMA wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mussa Yona akipima afya baada ya kupata elimu ya afya na upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza, VVU na UKIMWI wakati wa Mkutano Mkuu wa Mwaka wa watumishi wa Ofisi hiyo uliofanyika Jijini Arusha.*



# Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yawapiga Msasa Watumishi Wapya

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendesha mafunzo kwa watumishi wapya yaliyolenga kuwajengea uwezo watumishi hao ili wazifahamu Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

Akizungumza kwa niaba ya Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Ofisi hiyo, ndugu James Kibamba alisema kuwa kupitia mafunzo haya watumishi walifundishwa mada mbalimbali ambazo zitawajengea msingi katika kutekeleza majukumu yao.

Mada zilizofundishwa ni pamoja na Muundo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 2009, Taratibu za uendeshaji wa Ofisi, Kanuni za Utumishi wa Umma na Marekebisho yake, Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 na Maadili ya Utumishi wa Umma.

Ameongeza kuwa dhumuni lingine la mafunzo hayo ni kuwawezesha watumishi hao kufahamu majukumu mbalimbali ya Ofisi hiyo ambayo ni kuratibu, kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yanayohusu Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Ndugu Kibamba aliongeza kuwa wana imani kubwa na watumishi hao kwa kuwa ujio wao katika Ofisi utasaidia kuongeza tija na ufanisi katika kuiletea matokeo chanya Serikali na kutimiza matarajio ya Serikali kwa wananchi.

Amewasisitiza watumishi wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuyapa uzito mkubwa mafunzo haya kwani kupitia mada zilizofundishwa wamejengewa uwezo wa kiutendaji na kuepuka makosa mbalimbali ya kiutumishi ambayo yangeweza kufanyika.

Watumishi hao pia walitakiwa kuwa huru kuuliza maswali kwa ufasaha katika maeneo yote muhimu ili waweze kuongeza uelewa katika maeneo yote yanayohusiana na utumishi wa umma.

*"Jisikieni huru kuuliza maswali na kuhakikisha kuwa mashaka yenu yote kuhusu masuala mbalimbali ya kiutumishi yanajibiwa,"* alisema ndugu Kibamba.



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu James Kibamba akifunga mafunzo elekezi kwa niaba ya Kaimu Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Mark Mulwambo kwa waajiriwa wapya wa Ofisi hiyo (hawapo pichani) kuhusu sheria, kanuni taratibu za utumishi wa umma wakati wa mafunzo yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Wakili wa Serikali Mkuu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu Reginald Makoko akitoa neno la shukrani kwa uongozi wa Ofisi hiyo kwa niaba ya watumishi wengine baada ya mafunzo elekezi yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*



*Watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Ofisi hiyo, ndugu James Kibamba (hayupo pichani) wakati wa mafunzo elekezi kwa watumishi wa umma yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*




*Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb) akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Njombe.*

# Ofisi Yashiriki Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia

Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inayoitwa, "Mama Samia Legal Aid Campaign" inatekelezwa na Wizara ya Katiba na Sheria. Kampeni hii ni endelevu kwa kipindi cha miaka mitatu tangu kuzinduliwa kwake mkoani Dodoma tarehe 27 Aprili, 2023 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb). Kampeni hiyo imepangwa kufanyika katika mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar na imejikita kwenye utoaji wa elimu ya kisheria kwa wananchi hususan katika masuala ya ukatili wa kijinsia, migogoro ya ardhi, mirathi, usuluhishi wa migogoro kwa njia mbadala na masuala yanayohusu haki za binadamu.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilishiriki katika kampeni hiyo mkoani Njombe ambayo ilifanyika kwenye viwanja vya Stendi ya Zamani kuanzia tarehe 26 Mei, 2024 hadi tarehe 4 Juni, 2024. Kampeni hiyo ilifunguliwa rasmi na Mhe. Dkt. Dotto Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Madini ikiwa na Kauli mbiu isemayo, "Msaada wa Kisheria kwa Haki, Usawa, Amani na Maendeleo."

Pamoja na utoaji wa msaada wa kisheria kwa

wananchi, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliweza kujitangaza kwa kuwaelimisha wadau na wananchi waliotembelea kwenye banda la maonesho ambapo walijenga uelewa kwao kuhusu dira, dhima, malengo, majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na inavyoendesha mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake. Pia, wadau walipewa taratibu za kufuata pale ambapo wanataka kuishtaki Serikali ambapo walielezwa kuwa wanapaswa kutoa notisi ya siku tisini (90) ambayo ni takwa la kisheria. Jumla ya watu 124 walipatiwa msaada wa kisheria katika Kampeni hiyo kupitia Ofsi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambapo wanaume walikuwa 27 na wanawake 97.

Pamoja na wadau mbalimbali waliohudhuria kwenye banda la maonesho na kupatiwa elimu ya msaada wa kisheria, vile vile viongozi mbalimbali walitembelea banda hilo ikiwemo Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria; Mhe. Jumanne Sagini, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria; na Bi. Mary Makondo; Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria.

Ushiriki wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye Kampeni hiyo umeonyesha wazi kwamba, Ofisi imekuwa mstari wa mbele katika kutekeleza na kutafsiri maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan yakuona si tu haki inapatikana bali inapatikana kwa wakati na kuwasaidia wananchi wanyonge. Zifuatazo ni faida ambazo Ofisi itachangia kwa jamii kwa kushiriki kwenye Kampeni hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Ofisi ni mmoja wa wadau muhimu kwenye mnyororo wa utoaji haki nchini, hivyo ushiriki wake kwenye Kampeni ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia utasaidia kuboresha upatikanaji wa haki kwa watu wa kipato cha chini ambao mara nyingi wanakosa fursa ya kupata msaada wa kisheria kutokana na gharama kubwa za kisheria;

(ii) Ofisi imetoa mchango na kutimiza lengo la Kampeni hiyo



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Jumanne Sagini (Mb) akitoa pongezi kwa Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali alipotembelea banda la Ofisi hiyo, Njombe*

la kujenga uelewa wa masuala ya kisheria kwa wananchi wa kawaida na hivyo kulinda na kukuza upatikanaji wa haki kwa wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria nchini;

(iii) Imesaidia kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu elimu ya sheria, masuala ya haki na wajibu; na misingi ya utawala bora;

(iv) Imechangia kuimarisha amani na utulivu kwa wananchi ambapo elimu ya sheria itasababisha kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na kuleta utengamano wa kisiasa hapa nchini kwakuwa wananchi walielimishwa namna ya kupata haki zao pale uhitaji unapotokea;

(v) Itapunguza uzalishaji wa kesi kwenye Mahakama kwani wananchi watafahamu taratibu nyingine za kiutawala za namna ya kushughulikia changamoto zao kuliko kukimbilia mahakamani kwa kila changamoto wanayokutana nayo; na

(vi) Itapunguza mrundikano wa kesi kwani mwananchi aliyeelimika kuhusu haki zake na sheria ni rahisi kujieleza mahakamani wakati shauri lake linapokuja mahakamani badala ya kuahirisha mashauri hayo bila sababu kwa ajili ya kuhofia kushindwa kujieleza.

Ofisi imetambua umuhimu wa kushiriki kwenye Kampeni hiyo kwa kuwa pamoja na kutoa elimu ya sheria kwa wananchi, vile vile ushiriki wa Ofisi ni sehemu ya kurudisha kwa jamii elimu, ujuzi na uzoefu ambao Ofisi inaupata kutokana na namna inavyofanya kazi katika Sekta ya Sheria. Pia, Ofisi itaendelea kushiriki kwenye Kampeni hiyo katika mikoa mbalimbali kadri Kampeni hiyo itakavyokuwa inatangazwa.

*Mwananchi akiwasilikiza Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali alipotembelea banda la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Njombe*



# Vyanzo na Mbinu za Kuendesha na Kupunguza Mashauri ya Serikali

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilianzishwa mwaka 2018 na kukasimiwa majukumu ya kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi. Katika kipindi cha miaka sita tangu kuanzishwa kwake, Ofisi imebaini changamoto mbali mbali ambazo zimejitokeza wakati wa uendeshaji wa mashauri. Changamoto zifuatazo zimeainishwa:-

(i) Baadhi ya taasisi za umma kutokuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo wakati wa kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wa umma hivyo kusababisha kufunguliwa kwa mashauri mengi ya kazi ambayo yangeweza kuepukwa endapo taratibu na sheria zingezingatiwa;

(ii) Baadhi ya taasisi zinazosimamia Sekta ya Ardhi kutozingatia taratibu za utwaaji wa maeneo na upimaji wa viwanja, malipo ya fidia na ugawaji wa viwanja;

(iii) Usimamizi hafifu wa kila hatua za mradi. Hivyo, kuleta changamoto za kupata ushahidi wa kujitosheleza wa uvunjifu wa masharti ya mikataba pale Serikali inaposhtakiwa au inapoamua kushtaki;

(iv) Ucheleweshaji wa kufanyia kazi malalamiko ya wawekezaji;

(v) Baadhi ya taasisi za Serikali kuvunja mikataba bila kushirikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hivyo kushindwa kufuata taratibu za kuvunja mikataba na kusababisha Serikali kushitakiwa; na

(vi) Kuchelewesha malipo kwa watoa huduma na wakandarasi ambapo baadhi ya taasisi za umma zinachelewa kufanya malipo kwa wakandarasi na watoa huduma kutokana na sababu mbalimbali na kupelekea Serikali kudaiwa madeni, riba na gharama za kuendesha kesi.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kupitia Hotuba ya Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende aliyoitoa kwenye Mafunzo ya Mawakili wa Serikali Mwaka 2024 aliishauri Serikali mbinu zifuatazo zifanyike ili kupunguza mashauri ya Serikali:-

i. Taasisi za umma zinakumbushwa kuzingatia sheria na taratibu katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwemo usimamizi wa mikataba na uvunjaji wa mikataba;

ii. Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iendelee kutoa elimu na miongozo kwa taasisi za umma ili kuzingatia sheria na kanuni wakati wa kuchukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wa umma;

iii. Taasisi zinazohusika kusimamia wawekezaji watekeleze jukumu hilo kwa kufanya ufuatiliaji wa karibu tangu wanapoingia mikataba na kipindi cha utekelezaji wa miradi hiyo ili kuepusha madai makubwa kwenye maeneo ambayo mwekezaji hajawekeza vya kutosha;

iv. Kuendelea kuboresha uratibu kwa kuwa na sehemu moja (one stop centre) ambayo mwekezaji atawasiliana na Serikali. Jambo hili litapunguza maelekezo tofauti na yanayokinzana ndani ya Serikali ambayo wakati mwingine yamekuwa yakitolewa na taasisi au Idara mbalimbali kwa wawekezaji;

v. Kuendelea kukumbusha Taasisi za Serikali kutunza nyaraka zote zinazotumika kwenye mawasiliano na wawekezaji au wadau mbalimbali ili kuepusha upotezaji wa taarifa;

vi. Kutoa elimu kwa watumishi wa umma kuhusu usimamizi wa mikataba ili kujenga uwezo wa kusimamia kwa umakini zaidi mikataba na miradi ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi;

vii. Kufanya ukaguzi wa kina kabla ya mwekezaji kuanza shughuli za kuomba kufanya uwekezaji (due diligence) ikiwa ni pamoja na kufahamu uwezo na uzoefu wa uwekezaji

anaotaka kufanya nchini; na

viii. Serikali iweke msisitizo kwenye utoaji wa mafunzo ya kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali.

Hivyo, mbinu hizo zikizingatiwa zitapunguza migogoro ya Serikali kwa kiasi kikubwa na kuiwezesha Serikali kuenenda kwa mujibu wa sheria kabla ya kuchukua hatua yoyote ya kisheria. Pia, kutaweka mazingira rafiki ya uwekezaji nchini kwakuwa migogoro ya uwekezaji inaweza kutatuliwa kwa njia ya maridhiano.



*Mawakili wa Serikali wakiwasikiliza wawezeshaji wa mada zilizotolewa wakati wa mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofayika Jijini Arusha.*



*Mawakili wa Serikali wakiwasikiliza wawezeshaji wa mada zilizotolewa wakati wa mafunzo kwa mawakili hao yaliyofayika Jijini Arusha.*

# Sheria Mpya za Uchaguzi na Nafasi ya Mawakili wa Serikali

Uchaguzi ni utaratibu uliowekwa na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwa ni njia ya wananchi kuwachagua viongozi watakaowawakilisha katika maeneo yao kuanzia madiwani katika ngazi ya kata, Wabunge katika ngazi ya jimbo na Rais katika ngazi ya kitaifa.

Mwaka 2024 na 2025 ni mwaka wa uchaguzi ambapo wananchi watatumia haki ya kupiga kura kwa mujibu wa Ibara ya 5 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Kwa upande mwingine, wananchi watatumia haki yao ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi kwa mujibu wa Ibara ya 21 ya Katiba kwa kugombea na kuchaguliwa na wananchi kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Sheria za Uchaguzi.

Itambulike kwamba suala la uchaguzi ni suala la mchakato na sio tukio la siku moja la kuchagua au kuchaguliwa na kutangaza matokeo. Suala la uchaguzi linahusu michakato ya ndani ya uchaguzi kwa vyama vya siasa, usajili wa wapiga kura, uboreshaji wa daftari la wapiga kura, utoaji wa fomu za kugombea nafasi mbalimbali, kampeni za kisiasa, uchaguzi na utangazaji wa matokeo. Hatua za uchaguzi zinaweza kusababisha uwepo wa mashauri yanayohusu uchaguzi na shauri linaweza kufunguliwa Mahakamani. Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa niaba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inawajibika kuitetea na kuiwakilisha Serikali Mahakamani. Uzoefu unaonesha kwamba shauri linaweza kufunguliwa dhidi ya Afisa au Ofisi yoyote ya Serikali ambayo inahusika moja kwa moja katika mchakato wa uchaguzi iwe ni wakati wa kampeni au kutangaza matokeo.

Mwaka 2024, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mamlaka yake chini ya Ibara 64 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga sheria mpya za uchaguzi. Utungaji wa sheria unaibua maboresho mbalimbali katika mchakato wa uchaguzi ambao ni muhimu sana kufahamika kwa wadau ikiwemo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali pamoja na Mawakili wa Serikali. Kwa kutambua umuhimu huo, Ofisi Wakili Mkuu wa Serikali iliandaa mafunzo jijini Arusha tarehe 20-22 Aprili, 2024 kwa lengo la kuwanoa Mawakili wa Serikali kuhusu sheria mpya za uchaguzi. Mada hii iliwasilishwa na Mhe. Jaji Emmanuel Kawishe, Jaji wa Mahakama Kuu, Kanda ya Mbeya pamoja na Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu, Mhe. Robert Makaramba.

Sheria Za Uchaguzi Kabla Ya Mwaka 2024.

Kwa ujumla sheria za uchaguzi zinapata msingi kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni sheria mama inayotoa haki ya kupiga kura, haki ya mtu kuchagua na kuchaguliwa, usajili wa wapiga kura, mipaka ya majimbo, sifa za kuchaguliwa kuwa Rais, Makamu wa Rais na Wabunge.

Kabla ya mwaka 2024, uchaguzi ulikuwa unasimamiwa na sheria nyingi ikiwemo; Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343; Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa; Sheria ya Gharama za Uchaguzi; Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji); na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya). Washiriki walipata wasaa wa kujifunza mfumo wa utatuzi wa migogoro ulivyokuwa kabla ya kutungwa kwa sheria mpya za uchaguzi za mwaka 2024.

Shauri la Kupita Bila Kupingwa kwa Mgombea.

Mahakama Kuu ya Tanzania, Masijala Kuu ya Dar es Salaam ilisikiliza Shauri la katiba namba 19 la mwaka 2021 kati ya Joran Lwehabura Bashange dhidi ya Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mleta shauri alidai kwamba kifungu cha 44 cha Sheria ya Taifa

ya Uchaguzi sura ya 343 na Kifungu cha 45 (2) na kifungu cha 13 cha Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2012 vimekiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika shauri hili, Mahakama ilibatilisha vifungu vilivyokuwa vinaruhusu mgombea kupita bila kupingwa na kutopigiwa kura na wananchi.

Kutungwa kwa Sheria Mpya za Uchaguzi.

Baada ya malalamiko ya wananchi kuwa mengi, Serikali iliamua kuchukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kurekebisha vifungu vilivyokuwa vinaruhusu mgombea kupita bila kupingwa kwa kupeleka muswada wa sheria Bungeni wenye lengo la kuondoa vifungu vilivyokuwa vinaruhusu mgombea kupita bila kupingwa. Muswada wa sheria ulijadiliwa na Wabunge na Sheria mpya zilitungwa na Bunge na kupitisha Sheria inayofuta Hukumu ya Mahakama iliyobatilisha vifungu hivyo na sheria hizo mpya ziliidhinishwa na Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Sheria zilizotungwa ni pamoja na; Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya Mwaka 2024, Sheria Na.1 ya Mwaka 2024; Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 2024, Sheria Na.2 ya mwaka 2024; na Sheria ya Vyama vya Siasa, 2024, Sheria Na. 3 ya Mwaka 2024.

Mambo Muhimu katika Sheria Mpya ya Uchaguzi.

Sheria mpya za uchaguzi zimepungua kwa kuweka masuala ya uchaguzi katika Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na.1 ya 2024; na Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya mwaka 2024. Sheria hii imefuta Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1979 kwa mujibu wa kifungu cha 167. Kimsingi, masuala mengi yameendelea kuwepo kama ilivyokuwa kwenye sheria zilizofutwa isipokuwa suala la mgombea kupita bila kupingwa. Kwa sasa mgombea huyo atatangazwa kama mgombea pekee na atatakiwa kupigiwa kura ya ndiyo au hapana. Hivyo, wananchi watatumia haki yao ya kumchagua kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Utaratibu huu umewekwa katika kifungu cha 54 kwa upande wa Wabunge na kifungu cha 66 kwa upande wa Madiwani katika Sheria Na. 1 ya Mwaka 2024.

Aidha, sheria ndogo zote zilizotungwa chini ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1979 ambazo bado zinatumika, zitachukuliwa kuwa zimetungwa chini ya Sheria hii hadi pale zitakapofutwa na Sheria hii au sheria ndogo zitakazotungwa chini ya Sheria hii. Hivyo ni muhimu kutambua kuwa sheria ndogo zote ambazo hazijafutwa zitaendelea kutumika licha ya uwepo wa Sheria Na. 1 ya Mwaka 2024 kwa mujibu wa kifungu cha 168(c).

Aidha, suala la Wakurugenzi kuendelea kusimamia uchaguzi, msimamo wa Mahakama ya Rufani katika Shauri la Rufaa Na. 138 la Mwaka 2019 kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wenzake dhidi ya Bob Chacha Wangwe unaendelea kuwa msimamo wa Sheria na Wakurugenzi wataendelea kusimamia uchaguzi. Utaratibu wa kupata wasimamizi wa Uchaguzi umewekwa bayana katika kifungu cha 6 cha Sheria Na. 1 ya Mwaka 2024. Ieleweke kuwa Tume ina uwezo wa kumteua mtumishi wa umma mwandamizi kuwa Msimamizi wa Uchaguzi kwa mujibu wa kifungu cha 6(1) cha Sheria Na. 1 ya Mwaka 2024. Aidha, Tume inaweza kumteua mtumishi wa umma kwa jina lake au cheo chake kuwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kwa mujibu wa Kifungu cha 6(2) cha Sheria hiyo.

Mfumo wa utatuzi wa migogoro umebaki kama ulivyo kwenye sheria za zamani za uchaguzi. Mahakama Kuu inaendelea kuwa na mamlaka ya utatuzi wa migogoro ya uchaguzi kwa nafasi ya Ubunge na wakati upande wa Madiwani unabaki kwenye Mahakama ya Hakimu Mkazi. Pia, msimamo wa kisheria kwamba matokeo ya nafasi ya Rais kutopingwa Mahakamani unaendelea kuwa ndio msimamo wa kisheria kuhusu uchaguzi wa nafasi ya Rais. Aidha, watu wenye sifa ya kupinga na kuwasilisha shauri la uchaguzi Mahakamani ni pamoja na mtu aliyepiga kura kihalali au alikuwa na haki ya kupiga kura katika uchaguzi ambao shauri linahusika; mtu anayedai kuwa alikuwa na haki ya kuteuliwa au kuchaguliwa katika uchaguzi huo; mtu anayedai kuwa alikuwa mgombea katika uchaguzi huo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 150 (1) cha Sheria Na. 1 ya

Mwaka 2024.

Utaratibu wa kuwa na Dhamana ya Gharama kwenye mashauri ya uchaguzi umeendelea kama ulivyokuwa kwenye Sheria za Uchaguzi za zamani. Msajili wa Mahakama hatapanga tarehe ya kusikilizwa kwa shauri lolote la uchaguzi isipokuwa kama mlalamikaji amelipa mahakamani dhamana ya gharama kiasi kisichozidi shilingi milioni tano kwa Wabunge na laki tano kwa Madiwani. Ushahidi unaohitajika ili shauri la uchaguzi liamuliwe kwa faida ya mlalamikaji ni kiwango cha kuiridhisha Mahakama. Kiwango kilichowekwa katika Shauri la Manju Salum Msambya dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Kifu Gulam Hussein Kifu, Shauri la Rufaa Na.2 la Mwaka 2002 kwamba suala la uchaguzi ni suala nyeti sana na kwamba kiwango cha kuthibitisha ni kile kisichoacha mashaka bado haijabatilishwa kama ilivyo kwa sasa kwenye mashauri ya kikatiba kati ya Mwanasheria Mkuu dhidi ya Dickson Paul Sanga, Shauri la Rufaa Na. 175 la Mwaka 2020.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliandaa mada kuhusu Sheria Mpya ya Uchaguzi kwa Mawakili wa Serikali ikiwa ni muendelezo wa jitihada za Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwajengea uwezo Mawakili hao ili waweze kuielewa na kujiandaa na mashauri ya uchaguzi kwa Mwaka 2024 na 2025.




*Jaji Mstaafu wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Robert Makaramba akitoa mada kuhusu taratibu za uendeshaji wa Mashauri ya Uchaguzi wakati wa mafunzo ya Mawakili wa Serikali jijini Arusha.*




*Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mhe. Emmanuel Kawishe akitoa mada kuhusu mabadiliko ya sheria za uchaguzi ya mwaka 2024 wakati wa mafunzo ya Mawakili wa Serikali jijini Arusha.*

# Wajibu na Majukumu ya Wakili wa Serikali

Wakili kwa kiswahili rahisi linamaanisha mwakilishi, mtetezi au msimamizi kwa niaba ya mtu mwingine kwa lengo la kumtetea au kufanya kazi kwa niaba yake. Kwa muktadha huo ni wazi kwamba tunapozungumzia Wakili wa Serikali kwa lugha nyepesi inamaanisha mtu anaye fanya kazi ya kuiwakilisha, kuitetea au kuisimamia Serikali.

Mbali na muktadha huo, neno Wakili wa Serikali imeelezwa kwa kirefu katika Kifungu cha 3 na Kifungu cha 24 cha Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268. Kwa ufupi na kwa tafsiri isiyo rasmi, Wakili wa Serikali anaweza kutambulika kuwa ni Mwanasheria aliyeajiriwa na Serikali katika upana wake kama ilivyofafanuliwa katika kifungu cha 16(4) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri dhidi ya Serikali, Sura ya 5 ambapo pamoja na mambo mengine Serikali inajumuisha Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma.

Mawakili wa Serikali ni kada muhimu katika kusimamia maslahi ya Taifa na ustawi wa wananchi wake. Msingi mkuu wa jukumu hili unatokana na Ibara ya 8(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 kama ilivyofanyiwa marejeo ambayo inatamka kwamba:

8.-(1) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia na haki ya kijamii na kwa hiyo:-

(a) wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii;

(b) lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi;

(c) Serikali itawajibika kwa wananchi; na

(d) wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali yao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.

Kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Tanzania, 1977 na sheria nyingine zilizopo, kazi na wajibu wa Mwanasheria wa Serikali kwa pamoja ni kuwawezesha viongozi, akiwemo Rais ambaye ni mkuu wa nchi, kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu; Spika ambaye ni kiongozi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Jaji Mkuu ambaye ni kiongozi wa Mahakama ya Rufani na Mkuu wa Mahakama ya Tanzania; kutekeleza madaraka yao ya kikatiba. Kwa muktadha huo, hakuna shaka kwamba Mawakili wa Serikali wanafanya kazi na mihimili mitatu tajwa hapo juu ambayo ni Serikali, Bunge na Mahakama. Fursa hii ni adhimu na ya heshima kwa Mawakili wa Serikali kutekeleza majukumu hayo ya kuiwakilisha Serikali na taasisi zake kwenye mashauri mbali mbali.

Mbali na wajibu walionao Mawakili wa Serikali kwa kuzingatia msingi wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vile vile Mawakili wana wajibu na majukumu ambayo yameainishwa kwenye sheria mbalimbali ambazo zinasimamia majukumu yao mahsusi ikiwemo sheria zifuatazo:

(i) Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act Cap. 268 R.E 2019);

(ii) Maadili ya Maafisa Sheria, Mawakili wa Serikali na Wanasheria (The Code of Ethics and Professional Conduct of Law Officers, State Attorney and Legal officers);

(iii) Sheria ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430 (The National Prosecutions Service Act [Cap. 430 R.E 2019];

(iv) Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mwongozo kwa Mawakili wa Serikali na Maafisa Sheria wa 2020 (The Attorney

General (Discharge of Duties) Guidelines for Practicing State Attorneys and Law Officers, 2020);

(v) Amri ya Marekebisho ya Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali [Office of the Attorney General (Re-structure) Order, 2018. (GN. No. 48 of 2018);

(vi) Tangazo la Serikali Na.49 la Mwaka 2018 la tarehe 13 Februari, 2018 la kuanzisha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; na

(vii) Tangazo la Serikali Na.50 la Mwaka 2018 la tarehe 13 Februari, 2018 la kuanzisha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Pamoja na sheria tajwa hapo juu, kwa kuwa Mawakili wa Serikali pia ni watumishi wa umma, wanatakiwa kuzingatia kanuni na maadili ya utumishi wa umma kama yalivyoainishwa katika sheria za utumishi wa umma zifuatazo:

(i) Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298;

(ii) Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003;

(ii) Kanuni za Maadili za Utumishi wa Umma (Public Service Disciplinary Code of Good Practice G.N 53/2007);

(iv) Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, 2009 (Standing Orders for the Public Service, GN 493/2009;

(v) Sheria ya Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma, Sura ya 398 (Public Leadership Code of Ethics [Cap. 398 R.E. 2002]) ambayo msingi wake ni Ibara ya 132 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;

(vi) Sheria ya Mawakili, Sura ya 341 (The Advocates Act (CAP. 341);

(vii) Kanuni za Maadili Kitaaluma na Mwenendo wa Mawakili za Mwaka 2018 (The Advocates (Professional Conduct and Etiquette) Regulations, 2018;

(xiii) Kanuni za Maadili na Mwenendo wa Watumishi katika Utumishi wa Umma (The Code of Ethics and Conduct for Public Service); na

(ix) Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Wajibu na Majukumu ya Ujumla ya Mawakili wa Serikali.

Kifungu cha 16 (1) cha Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 kinampa Wakili wa Serikali wajibu wa kutekeleza majukumu yote ya kikatiba ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa katika sheria hiyo.

Vilevile kwa mujibu wa Kifungu cha 3 (1) kikisomwa pamoja na Kifungu 3(2) cha Sheria ya Mawakili (Sura ya 341) Wakili wa Serikali anatambulika kama Wakili kutokana na wadhifa wake. Nafasi hii inamwongezea wajibu kwa kuwa Kifungu cha 106 (1) cha Kanuni za (Kanuni za Maadili Kitaaluma na Mwenendo wa Mawakili za mwaka 2018) kinatarajia Wakili anayefanya kazi kwenye Sekta ya Umma kuwajibika kwa kiwango sawa na Mawakili wa kujitegemea. Aidha, Kanuni hizo zinatoa wajibu zaidi kwenye maeneo mbali mbali kama vile wajibu wa kudumisha na kuboresha haki, wajibu kwenye taaluma, wajibu kwa Mahakama na wajibu kwa wanasheria wenzake.

Vilevile, Wakili wa Serikali kwa nafasi yake kama Mtanzania anao wajibu wa kushiriki kujenga uchumi wa nchi kwa kuzingatia malengo na mikakati iliyopo katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka Mitano 2021/22–2025/26 kwa ajili ya ya kujenga uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu. Ili kufanikisha uchumi shindani, moja ya misingi muhimu ni kuwepo kwa mazingira ya amani, usalama, umoja, utawala bora na utawala wa sheria. Misingi hiyo imejengwa ndani ya Katiba, Sheria, Miongozo na Kanuni zinazowaongoza Mawakili wa Serikali ili kupiga hatua katika nyanja ya maendeleo ya uchumi, kijamii na kisiasa.

Utekelezaji wa malengo hayo pia unashabihiana na matakwa ya Sura ya Sita, Ibara ya 120 (a – l) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 ambayo inatekelezwa kwa kutengewa fedha kila mwaka. Matokeo ya utekelezaji yatakuwa ni kupungua kwa mrundikano wa kesi mahakamani, utoaji wa msaada wa kisheria kwa wananchi, kusogeza huduma karibu na wananchi na kupatikana kwa huduma bora za sheria kwa wakati na kwa gharama nafuu ili kuharakisha upatikanaji haki

nchini.

Mawakili wa Serikali wanasimamia shughuli za Divisheni na Vitengo kwenye Wizara, Idara na Taasisi za Serikali kwa mujibu wa miundo inayoanzisha au kusimamia Taasisi hizo. Pamoja na kwamba majukumu ya kila taasisi yanaanzishwa kwa mujibu wa sheria au hati (Instrument) inayoanzisha taasisi husika, majukumu ya utoaji huduma za kisheria yanafanana kwa taasisi zote. Majukumu hayo ni yafuatayo:-

(i) Kutoa ushauri na utaalam wa kisheria kwa mamlaka husika kwenye masuala mbalimbali ikiwemo utoaji wa ushauri kwa waajiri katika kushughulikia masuala ya ajira na nidhamu ili kuiepusha Serikali kupata hasara na kulipa fidia kwa watumishi wanaoajiriwa na kusimamishwa au kufukuzwa kazi bila kuzingatia sheria, taratibu na miongozo iliyopo;

(ii) Kuandaa na kupitia nyaraka mbalimbali za kisheria kama vile Mikataba, Hati za Makubaliano, Matangazo ya Serikali kulingana na Miongozo inayotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

(iii) Kuchambua nyaraka za mapendekezo / maandiko ya kisheria;

(iv) Kufanya majadiliano kuhusu mikataba na makubaliano mbalimbali yanayoingiwa na Taasisi kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya kusimamia utekelezaji wa mikataba ili kuongeza tija na ufanisi;

(v) Kuendesha kesi za madai na usuluhishi kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kuhakikisha migogoro inapojitokeza inashughulikiwa kwa haraka kwa njia za usuluhishi au majadiliano ili kupunguza uzalishaji wa mashauri;

(vi) Kuandaa nyaraka za mahakama;

(vii) Kuandaa rasimu za kanuni na mapendekezo ya utungaji au marekebisho ya sheria kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria;

(viii) Kuratibu na kusimamia watendaji waliopo chini ya Idara na Vitengo husika;

(ix) Kuratibu shughuli za Bodi (kwa kutegemea muundo wa Taasisi husika);

(x) Kuwa tayari kufanya kazi nyingine watakazopangiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakili Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka;

(xi) kubainisha maeneo yanayohitaji kujengewa uwezo ili kutekeleza majukumu yao vyema na kwa weledi; kuendelea kufanya tafiti katika maeneo mapya na ya kimkakati na kutoa matokeo ya tafiti hizo kwa wakati; na

(xii) Kutunza siri za Taasisi zao.

Utekelezaji wa majukumu haya yote unawahitaji Mawakili wa Serikali kuzingatia masharti ya Katiba, Sheria, Kanuni, maadili, uzalendo, weledi pamoja na miongozo mbalimbali iliyopo ya Mawakili wa Serikali ambayo ni nyenzo muhimu kwa maendeleo ya Taifa ikiwemo kuongoza kwa kuonesha mfano. Kwa mujibu wa Sheria, Wakili wa Serikali ni Wakili wa umma, hapaswi kuwa na mipaka finyu katika maeneo ya kutekeleza majukumu yake kwa Taifa.

Endapo maadili yatazingatiwa, tija kwa Serikali itaongezeka kupitia ushauri wa kisheria unaotolewa, majadiliano yatakayofanyika kwa nia njema, mikataba yenye maslahi mapana kwa nchi itakayoingiwa itasaidia kuibua miradi mbalimbali kwa maendeleo ya Taifa, sheria zitakazoandaliwa na kuzingatiwa na wananchi zitachochea kuwepo kwa maendeleo, amani na usalama, mashauri dhidi ya Serikali yatapungua, vitendo visivyo vya kimaadili kama vile rushwa vitapungua au havitakuwepo.

*Mawakili wa Serikali ni kada muhimu katika kusimamia maslahi ya Taifa na ustawi wa wananchi wake. Msingi mkuu wa jukumu hili unatokana na Ibara ya 8(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 kama ilivyofanyiwa marejeo.*




*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Jumanne Sagini (Mb), (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali (waliosimama nyuma) wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya kufungua mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.*




*Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali (waliosimama nyuma) wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kufunga mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Arusha.*




*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Prisca Ulomi akitoa mada kuhusu namna ya kuzungumza na mahusiano (The Art of Public Speaking & PR) mbele ya halaiki kwa Menejimenti na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwenye mkutano wa Ofisi hiyo uliofanyika jijini Arusha.*



*Mawakili wa Serikali wakiwasikiliza wawezeshaji wa mada zilizotolewa wakati wa mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofayika Jijini Arusha.*

# Serikali Yashinda Mashauri Ndani na Nje Ya Nchi

Hivi karibuni, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imejitokeza kwenye vichwa vya habari vya magazeti, runinga, redio na mitandao ya kijamii kwa umahiri wa kazi zake kwa kushinda mashauri za mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi na kuokoa fedha ambazo endapo Serikali ingeshindwa kesi hizo ingeadhibiwa kwa kulipa fedha hizo na hivyo kuathiri mapato ya Serikali ambayo yangetumika kutoa huduma kwa wananchi na kuleta maendeleo kwa taifa.

Mashauri ya usuluhishi kama yalivyo mashauri mengine, yana asili ya madai yanayotokana na mikataba au makubaliano baina ya pande mbili au zaidi ambapo wao wenyewe wameridhia na kuweka kipengele kinachotaka mgogoro unapotokea baina yao ufanyike kwa njia ya usuluhishi. Usuluhishi unaweza kufanyika ndani au nje ya nchi kulingana na makubaliano ya pande zilizopo katika Mkataba husika.

Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imefanikiwa kushinda na kuokoa kiasi kikubwa cha fedha kwenye mashauri mbali mbali ya usuluhishi yaliyofanyika ndani ya nchi kama ifuatavyo:-

i). Shauri la kupinga mkataba wa uwekezaji katika Bandari ya Dar es salaam katika Mahakama ya Tanzania, Mbeya na shauri la kupinga uwekezaji katika kiwanda cha Saruji, Tanga. Mashauri haya yalihusisha miradi ambayo ina uwekezaji mkubwa ambapo Serikali ingeshindwa uwekezaji huo usingeweza kufanyika;

ii). Shauri baina ya M/S Mavondo's Co. dhidi ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro. Shauri hili linatokana na mkataba wa ujenzi wa eneo la kupokea wageni ambapo mkandarasi hakukamilisha kwa viwango walivyokubaliana. Hivyo, Ngorongoro kutaka kurudishiwa fedha zilizolipwa kwa mkandarasi ambapo mkandarasi hakuridhia na kuwasilisha mgogoro huo kwa Taasisi ya Usuluhishi Tanzania (TIArb) ambayo ilisikiliza mgogoro huo, na madai ya mkandarasi kutupiliwa mbali na kuiwezesha Serikali kuokoa kiasi cha shilingi za Tanzania 1,025,631,512.64;

iii). Shauri kati ya Wizara ya Elimu dhidi ya Climate Consultant Limited ambapo shauri hili linatokana na mkataba wa usambazaji wa vifaa vya TEHAMA. Shauri hili limehitimishwa kwa njia ya majadiliano baada ya mzabuni kukubali kwamba atailipa Serikali shilingi za Tanzania 141,649,254.27 na makubaliano haya yamefanyika kwa kusaini hati ya maridhiano; na

iv) Shauri Na. 231/2019 la TANESCO dhidi ya Intertrade Commercial Services. Shauri hili linatokana na kuvunjika kwa mkataba wa kusambaza mita za umeme kati ya TANESCO na Kampuni hiyo. Serikali ilishinda shauri hili na kuokoa dola za Marekani 3,624,723.5 na shilingi za Tanzania 147,441,546.

Mashauri tajwa hapo juu ni baadhi ya mashauri ambayo Serikali imeshinda ambapo yapo mashauri mengine mengi ambayo Serikali imeokoa fedha nyingi kupitia majadiliano ya na mengine kushinda kupitia hukumu za Mahakama.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendelea kuweka nguvu katika kuwekeza kwa Mawakili wa Serikali ili kuwapa uwezo wa kiushindani katika kuendesha mashauri kuongeza kasi ya mafanikio. Pamoja na kushinda mashauri ya ndani ya nchi, Pia Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeendelea kushinda mashauri ya nje ya nchi kama ifuatavyo:-

i). Shauri baina ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) dhidi ya Kampuni ya Alchemist Energy Trading DMCC ambapo Serikali ilishinda zaidi ya dola za Marekani millioni 14.4 sawa na takriban shilingi bilioni 36 kupitia uamuzi wa Baraza la Kimataifa la Biashara (International Chamber of Commerce-ICC).

Ushindi wa mashauri tajwa hapo juu ya usuluhushi ndani na nje ya nchi yanatokana na ueledi, bidii, juhudi, maarifa na uzalendo wa Mawakili wa Serikali kwa kuwa nguzo na chachu iliyoleta mafanikio hayo katika mashauri. Hivyo, Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo na kuwanoa Mawakili ili wawe mahiri zaidi katika kuendesha mashauri kwa niaba ya Serikali na taasisi zake.

# Zunda Achaguliwa Mfanyakazi Hodari wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali



**Athumani Adam Zunda**
*Afisa Kumbukumbu*

Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imemchagua ndugu Athumani Adam Zunda kuwa mfanyakazi hodari wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kikao kilichofanyika katika ukumbi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dar es Salaam.

Akizungumza mara baada ya uchaguzi huo, Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu, ndugu James Kibamba alisema kuwa uchaguzi huo umezingazitia sifa na vigezo vilivyowekwa ambavyo mtumishi anatakiwa kuvifikia ili waweze kuchaguliwa kuwa wafanyakazi hodari.

Kiabamba amewataka watumishi wa Ofisi hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii, weledi na uadilifu kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma katika kuwahudumia wananchi kwa ustawi wa taifa ili kuhakikisha wanaiwezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu yake kwa wakati.

Aidha, Kibamba amefafanua kuwa Zunda ni mtumishi aliyestahili kuwa mfanyakazi Hodari kwa kuwa amekuwa akitekeleza majukumu yake kwa umahiri mkubwa katika kuwahudumia wananchi na watumishi wenzake wanaofika kupata huduma Ofisi bila upendeleo na kwa wakati.

Ameongeza kuwa ushindi wa Zunda ni funzo kwa vijana wengine waliopo kazini na ametoa wito kwa viongozi kuendelea kuwaamini vijana kwa kuwa ni nguvu kazi ya taifa na wanafanya kazi kwa bidi ili kuhakikisha wanaliletea taifa hili maendeleo.

Kwa upande wake, Zunda amewashukuru viongozi kwa kuwaongoza watumishi wote na kusimamia maadili, kufanya kazi kwa bidii na weledi katika kulitumikia taifa jambo ambalo limemfanya kuwa mfanyakazi hodari wa Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

Aidha, amewashukuru wafanyakazi wenzake kwa kumpa ushindi wa kishindo na kuahidi kuendelea kutoa huduma bora kwa watumishi wa umma na wananchi wanaopatiwa huduma katika Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

“Kitendo cha kuchaguliwa kuwa mfanyakazi bora kitaendelea kuniongezea nguvu na kujenga taswira nzuri zaidi ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na kimenipa ari, motisha na hamasa ya kufanya kazi kwa bidi,” alisema Zunda.

Pia, Zunda amewaahidi Menejimenti na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuwa ataendelea kuwa mwadilifu na mchapa kazi katika kipindi chote cha utumishi wake ili kuendelea kuwa mfano kwa watumishi wenzake hasa watumishi wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Uchaguzi wa mfanyakazi hodari wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ulitanguliwa na uchaguzi wa wafanyakazi bora kutoka Idara na Vitengo vya Ofisi hiyo ambapo kila Idara na Kitengo ilipata mfanyakazi bora na baadae watumishi hao walipigiwa kura na Menejimenti na Zunda aliibuka kidedea kwa kuchaguliwa kuwa mfanyakazi hodari wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 203/24. Kongole kwako Zunda!

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

| | |
|---|---|
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1902<br>41218 DODOMA<br>Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)<br>Barua pepe: dodoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 130<br>31101 MUSOMA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mara@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 1280<br>63114 MTWARA<br>Maadili House<br>Barua pepe: mtwara@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 394<br>33101 MWANZA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: mwanza@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 595<br>51108 IRINGA<br>Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa<br>Barua pepe: iringa@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 106<br>35102 BUKOBA<br>Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali<br>Barua pepe: kagera@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 564<br>57101 SONGEA<br>Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 43<br>37101 SHINYANGA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 60<br>21101 TANGA<br>Jengo la Mkonge<br>Barua pepe: tanga@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 119<br>45112 TABORA<br>Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa<br>Barua pepe: tabora@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 202<br>25101 MOSHI<br>Jengo la TRA Moshi<br>Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 690<br>55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi<br>Jengo la Ukaguzi, Gorofa ya pili<br>Barua pepe: rukwa@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 66<br>23101 ARUSHA<br>Jengo la AICC, Arusha<br>Barua pepe: arusha@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 710<br>53107 MBEYA<br>Jengo la Madini<br>Barua pepe: mbeya@osg.go.tz |
| OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>S. L. P 172<br>47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,<br>Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.<br>Barua pepe: kigoma@osg.go.tz | OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI<br>Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne<br>MOROGORO, Barabara ya zamani DSM<br>Barua pepe: morogoro@osg.go.tz |